# WIZARA YA MAJI

## MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI DODOMA (DUWASA)

# HALI YA UTOAJI HUDUMA, CHANGAMOTO NA MIPANGO YA UBORESHAJI WA MAJI JIJINI DODOMA.

**(Taarifa kwa Mkuu wa Mkoa)**

Imeandaliwa na:
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA)
S.L.P 431,
**DODOMA**

**Juni, 2020**

**YALIYOMO**


| NA. | MAELEZO | KURASA |
| --- | --- | --- |
| 1.0 | UTANGULIZI…………………………………………………...………… | 2 |
| 2.0 | HISTORIA FUPI YA UPATIKANAJI WA MAJI JIJINI DODOMA…… | 5 |
| 3.0 | HALI YA SASA YA HUDUMA YA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA JIJINI DODOMA……………………………………………… | 6 |
| 4.0 | UCHAKATAJI WA ANKARA, USAMBAZAJI NA MALIPO (MAKUSANYO)……………………………………………………………… | 11 |
| 5.0 | CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI DUWASA …………………….......…. | 12 |
| 6.0 | MIPANGO YA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA JIJINI DODOMA…………………………… | 13 |
| 7.0 | HITIMISHO…………………………………………………….....……… | 16 |

## TAARIFA YA UTENDAJIKAZI WA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI DODOMA (DUWASA) KATIKA UTOAJI WA HUDUMA ZA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA JIJINI DODOMA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 DODOMA

Mji wa Dodoma ambao ni Makao Makuu ya Tanzania upo kilometa zipatazo 450 Magharibi mwa mji mkuu wa kibiashara wa Dar es Salaam. Mkoa huu upo katika mwinuko wa meta kati ya 1030 hadi 1320 kutoka usawa wa bahari. Aidha, unapatikana katika latitudo ya $6^{o}00'$ Kusini na longitude $35^{0}45'$ Mashariki.

### 1.2 DUWASA

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ilianzishwa mwezi Julai, 1998 kwa mujibu wa kifungu na 3(1) cha sheria No.8 ya mwaka 1997 ambayo ilifanyiwa mabadiliko kwa sheria Na. 12 ya mwaka 2009 pamoja na sheria namba 5 ya mwaka 2019 ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira. Jukumu la msingi la DUWASA ni kutoa huduma endelevu ya usambazaji Majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi wa Jiji la Dodoma. Aidha, katika kipindi cha hivi karibuni, DUWASA imeongezewa eneo la utendajikazi kujumuisha maeneo ya Miji ya Bahi, Kongwa na Chamwino.

DUWASA ilianzishwa ikiwa moja ya Mamlaka ya daraja ‘C’ ikitegemea ruzuku ya Serikali (Wizara ya Maji) katika uendeshaji hasa gharama za umeme na mishahara ya watumishi. Hata hivyo, ilipanda kutoka daraja ‘C’ hadi ‘A’ mnamo mwaka 2003 na hivyo kujitegemea kwa asilimia mia (100%) katika gharama za uendeshaji na sehemu ya uwekezaji.

### 1.3 DIRA (*VISION*) YA DUWASA

Kuwa Mamlaka yenye ufanisi wa hali ya juu katika utoaji wa huduma ya majisafi na salama na usafi wa mazingira katika hali endelevu.

### 1.4 DHIMA (*MISSION*)YA DUWASA

Utoaji wa huduma ya majisafi, salama na ya uhakika na usafi wa mazingira kwa wateja wa Mamlaka waliopo Jijini Dodoma Pamoja na maeneo yaliyoongezwa kwa ufanisi wa hali ya juu, kuwa na watumishi wenye shauku, bidii ya kazi na wanaojituma, kutumia teknolojia sahihi inayokubaliana na mazingira na kuendelea kujibidiisha zaidi ili kuongeza ufanisi na tija.

## 1.5 MUUNDO WA UTAWALA WA DUWASA


**(i) Bodi:**

DUWASA inafanya kazi chini ya Bodi ambayo wajumbe wake huchaguliwa na Waziri mwenye dhamana ya maji. Wajumbe hao huwakilisha makundi mbalimbali kama ifuatavyo:

- Mwenyekiti wa Bodi
- Mjumbe anayewakilisha jumuia ya wafanyabiashara
- Mkurugenzi wa Manispaa anayeingia kwa wadhifa wake.
- Mjumbe mwakilishi wa Serikali ya Mkoa
- Mjumbe anayewakilisha watumiaji wa maji majumbani
- Mjumbe anayewakilisha madiwani
- Mjumbe anayewakilisha wanawake
- Mjumbe anayewakilisha Wizara ya Maji
- Mjumbe anayewakilisha watumiaji wakubwa wa maji.
- Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ambaye ni Katibu wa Bodi.

**(ii) Menejimenti:**

Shughuli za kila siku za Mamlaka husimamiwa na Menejimenti inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji anayesaidiwa kwa karibu na Idara kuu tatu za Ufundi, Biashara na Fedha na Utawala pamoja na vitengo vitano (5) vinavyo ripoti kwa Mkurugenzi Mtendaji vya Manunuzi, Sheria, Uhusiano, Ukaguzi wa Ndani na Usimamizi wa Mifumo. Kwa ujumla, kufikia Juni, 2020, DUWASA ilikuwa na watumishi 195 katika kada mbalimbali (Wanaume 149 na Wanawake 45). Muundo wa DUWASA kwa ufupi umeoneshwa katika *Organisation chart* hapa chini;




## 1.6 Majukumu ya DUWASA

Kazi na Majukumu ya DUWASA kwa mujibu wa sheria namba 5 ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, kifungu cha 20(a-l) ni kama ifuatavyo:

(a) Kutoa huduma ya maji kwa wananchi kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa kuhusiana na utunzaji wa vyanzo vya maji, ubora wa maji pamoja na mazingira

(b) Kutoa huduma endelevu ya maji kwa matumizi na ubora unaokubalika kisheria pamoja na kufanya upimaji wa maji yanayosambazwa mara kwa mara kama ilivyoelezwa kwenye kanuni za ubora wa maji

(c) Kuendeleza na kufanya matengenezo ya miundombinu ya majisafi na majitaka

(d) Kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji

(e) Kuishauri Serikali juu ya miundo ya sera, miongozo na sheria kuhusiana na viwango vya huduma ya maji.

(f) Kupanga na kutekeleza miradi mipya ya majisafi na Majitaka

(g) Kuelimisha na kuipatia taarifa jamii kuhusiana na maji salama, uhifadhi wa maji, usafi wa mazingira na mengine yanayohusiana na hayo.

(h) Kushirikiana na Serikali za mitaa kwenye masuala yanayohusu huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na upanuzi wa mitandao ya maji kwa maeneo yanayoendelezwa.

(i) Kukusanya maduhuli na ada mbalimbali zinazohusiana na huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira pamoja na ada yoyote ya mdhibiti wa huduma za maji na Nishati (EWURA).

(j) Kupendekeza viwango vya malipo ya huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa EWURA.

(k) Kuweka vivutio vitakavyowezesha wateja kutumia huduma ya maji kwa urahisi zaidi.

(l) Kuingia mikataba au makubaliano ambayo Bodi ya Wakurugenzi imejiridhisha kuwa ni ya manufaa kwa Mamlaka na kuiidhinisha kwa mujibu wa sheria.

## 2.0 HISTORIA FUPI YA UPATIKANAJI WA MAJI JIJINI DODOMA.

Kabla ya mwaka 1987, huduma ya majisafi mjini Dodoma ilikuwa chini ya Mhandisi wa Maji wa Mkoa (*Regional Water Engineer*) ikiwa na jukumu la kusambaza huduma ya majisafi kwa wakazi wa Mjini Dodoma. Kuanzia mwaka 1987 jukumu la usambazaji wa huduma ya majisafi lilikuwa chini ya Idara ya Maji iliyokuwa chini ya ofisi ya Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa ambapo gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uwekezaji ziligharamiwa na Serikali Kuu na huduma ya maji ilikuwa ikitolewa bila ya kuwa na msisitizo wa kuilipia kutoka kwa watumiaji. Baadae mwaka 1998 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ilianzishwa kusimamia jukumu la utoaji wa huduma za majisafi na uondoshaji majitaka.

Kufikia mwaka 2002, hali ya maji mjini Dodoma haikuwa ya kuridhisha kutokana na kuwepo kwa migao mikali ya huduma ya majisafi. Migao hiyo ilifanya baadhi ya maeneo kupata maji mara moja kila baada ya wiki mbili tena kwa muda mfupi sana na mengine kutopata kabisa.

Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo ya njia ya bomba kuu la kusafirishia maji kati ya Mzakwe na Mjini. Eneo hilo lilijulikana kama ukanda wa kijani (*green belt*). Katika eneo hili, asilimia 80 ya maji yaliyokuwa yakizalishwa yaliishia katika matumizi ya kilimo cha mizabibu, bustani, migomba n.k. Kutokana na mfumo wa kulipia *flat rate* uliokuwepo hapo zamani, matumizi ya maji kwa umwagiliaji katika eneo hili yalikuwa makubwa na yasiyo na kiasi.

Hali hii ya migao mikali ilitishia ustawi wa mji kutokana na wawekezaji wengi kutotaka kuwekeza Dodoma.

Mara baada ya DUWASA kuanzishwa, na kwa msaada wa uongozi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ya Mkuu wa Wilaya, ilianza mikakati ya kuzuia matumizi ya majisafi kwa kilimo kisicho na tija. Aidha, ilianza mpango wa kufunga mita kwa watumiaji wote wa maji ili mteja alipie huduma ya maji

kulingana na matumizi yake badala ya mfumo wa *flat rate*. Ufungaji mita kwa wateja wote (*universal metering)* ulianza mwaka 2001 na kukamilika mwaka 2003.

Kukamilika kwa hatua hizo kulisaidia kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa mjini Dodoma ambapo migao ya maji ilikoma, na maeneo yote yaliyokuwa na mitandao lakini hayapati maji yalianza kupata maji ya uhakika muda wote.

DUWASA ilipoanzishwa mwaka 1998, uwezo wa uzalishaji maji kutoka katika chanzo cha Mzakwe ulikuwa ni meta za Ujazo 24,000 tu. Pia DUWASA ilirithi jumla ya wateja 4,800 wa majisafi, na hapakuwa na wateja wa majitaka kwa wakati huo kwani huduma hiyo ya uondoshaji majitaka ilikuwa ikitolewa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao makuu (CDA). Makusanyo ya maduhuli yalikuwa wastani wa Tsh. 14m/- tu kwa mwezi.

## 3.0 HALI YA HUDUMA YA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA JIJINI DODOMA

### 3.1 Huduma ya majisafi

#### 3.1.1 Mahitaji ya maji

Kwa mujibu wa stadi mpya (2020) ambayo imefanywa na Mhandisi Mshauri *Norplan-GiBB Joint Venture*, mahitaji ya maji Jijini Dodoma kwa sasa ni meta za ujazo 103,608 kwa siku (hii ni pamoja na maeneo yaliyokuwa vijijini ambayo DUWASA ilikuwa haiyahudumii). Mahitaji hayo yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia mita za ujazo 417,000 kwa siku miaka 30 ijayo (hadi mwaka 2051).

#### 3.1.2 Vyanzo na uwezo wa Uzalishaji maji

Chanzo pekee cha uzalishaji maji kwa matumizi ya wakazi wa mji wa Dodoma ni visima virefu vilivyochimbwa katika bonde la Makutupora. Bonde hili lipo takribani kilomita 30 kutoka mjini Dodoma. Jumla ya visima vya uzalishaji maji 24 na visima vitano (5) vya kuchunguza mwenendo wa maji ardhini (*observation boreholes*) vimechimbwa katika bonde hili. Uwezo wa visima vilivyopo kwa sasa pamoja na uwezo wa usafirishaji maji ni meta za ujazo zipatazo 61,500$m^3$ kwa siku.

Uwezo uliopo wa uzalishaji maji Mzakwe umefikiwa mwaka 2015 baada ya uwekezaji mkubwa wa mradi wa kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi kwa wakazi wa mjini Dodoma. Mradi huo uliongeza uwezo wa uzalishaji na usafirishaji wa maji kutoka kwenye chanzo (Mzakwe) kutoka wastani wa mita za ujazo 32,000 kwa siku hadi kufikia mita za ujazo 61,500 kwa siku.

### 3.1.3 Uzalishaji halisi

Hivi sasa DUWASA inazalisha, kusafirisha na kusambaza wastani wa meta za ujazo 55,000 kwa siku sawa na takribani asilimia 90 (90%) ya uwezo wa chanzo na siku za karibuni itafikia asilimia zaidi ya 95 baada ya kufunga pampu zaidi. Aidha, kuna chanzo cha maji cha Ihumwa chenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 2,700 kwa siku na kinatumika katika mji wa serikali Mtumba pamoja na mtaa wa Ihumwa. Pia kuna chanzo cha maji cha Iyumbu chenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 2,400 kwa siku kinachotumika Chuo Kikuu cha Dodoma (*Colleges* za Elimu na Tiba), Hospitali ya Benjamini Mkapa na Kijiji cha Nghong'onha.

### 3.1.4 Upungufu wa Maji uliopo

*Study* iliyofanywa na *Norplan-GiBB Jv* mwaka 2019 imeonesha uwepo wa upungu wa maji wa mita za ujazo 37,000 kwa siku baada ya kulinganisha vyanzo vilivyopo (66,600$m^3$/day) na mahitaji halisi ya maji (103,600$m^3$/day).

### 3.1.5 Utunzaji wa chanzo cha maji

Eneo lenye visima (*well field*) katika Bonde la Makutupora lina ukubwa wa 5,850Ha. Mnamo mwaka 1996, Wizara ya Maji ilifanya utafiti na kubaini kuanza kuchafuliwa kwa chanzo cha maji cha Makutupora kutokana na shughuli za kibinadamu zilizokuwa zinafanyika kama vile kilimo, ufugaji na ukataji miti.

Kufuatia hali hii, mwaka 2000 Serikali ilifanya tathmini ya kulipia fidia wananchi waliokuwa wanaishi eneo la Makutupora na baadaye mnamo mwaka 2002 ililipa fidia ya jumla ya Tsh. 590m/- kwa kaya 2,048 zilizokuwa zikiishi ndani ya Bonde katika vijiji vya Mzakwe, Gawaye, Mchemwa na Mamba. Mnamo mwaka 2007, Serikali ilitekeleza uamuzi wa kuzihamisha kaya hizo kwa nguvu baada ya kutotaka kuondoka kwa hiyari baada ya kulipwa fidia.

Aidha, katika kuhakikisha eneo hili lenye chanzo cha maji linatunzwa na haliingiliwi na shughuli za binadamu, Mnamo tarehe 21/09/2012, Waziri mwenye dhamana ya sekta ya maji, kupitia Gazeti la Serikali Na. 302, alilitangaza Bonde la Makutupora kuwa ni eneo Tengefu/Lililohifadhiwa na hivyo kuzuia shughuli zote za kibinadamu kufanyika katika eneo hilo.

Kwa sasa ulinzi na utunzaji wa chanzo hiki unafanyika kwa ushirikiano na Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa cha Makutupora, Ofisi ya Bonde la Wami/Ruvu na DUWASA.

### 3.1.6 Usafirishaji na Usambazaji maji mjini

Maji yanaposukumwa kutoka visimani hukusanywa kwenye matanki mawili yenye ujazo wa $680m^3$ na $800m^3$ yaliyopo Mzakwe. Ndani ya matanki hayo, maji hutibiwa kwa kutumia *chlorine* (*Chlorination*) iliyo katika mfumo wa *Calcium Hypochlorite*. Baada ya kutibiwa, maji huruhusiwa kuingia kwenye vituo vya kusukuma (kusafirisha) maji (*pumping stations*) kwenda mjini.

Kuna mabomba makuu mawili ya kusafirishia maji *(transmission mains)* kutoka kwenye chanzo eneo la Mzakwe kuja mjini yenye vipenyo vya mm 600 (inchi 24) kila moja. Mabomba hayo yana uwezo wa kusafirisha zaidi ya mita za ujazo 60,000 kwa siku kwa pamoja. Aidha, kuna vituo wiwili vikubwa vya kusukuma maji kutoka Mzakwe vinavyoweza kusukuma zaidi ya mita za ujazo 60,000 kwa siku.

Mtandao wa kusambazia majisafi kwa sasa una jumla ya urefu wa kilomita zipatazo 574 (Juni, 2020). Mtandao huu pia unajumuisha matenki makubwa mawili yenye ukubwa wa meta za ujazo 36,000 kila moja pamoja na matenki mengine manane (8) yanayotumika kuhifadhi na kusambaza maji yenye jumla ya meta za ujazo 20,030 hivyo kufanya jumla ya matenki yote kuwa na ujazo wa 90,470. Aidha, kuna matanki matatu yenye ujazo wa jumla ya $12,000m^3$ katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mtandao huu pia unajumuisha vituo sita (6) vya kusukumia maji.


Kwa sasa takribani asilimia 80 ya wakazi wa mjini Dodoma wanaokaribia kufikia 500,000 wanapata maji ya DUWASA. Hata hivyo, kufuatia ujio wa Serikali Makao Makuu - Dodoma, Mji wa Dodoma umekuwa ukipanuka kwa kasi na hivyo uhitaji wa kusogeza huduma za majisafi na majitaka kuongezeka.




*Tanki la kuhifadhi maji Imagi (kushoto) na kituo cha kusukuma maji Kilimani (kuulia).*

Hadi sasa, DUWASA ina jumla ya maunganisho (wateja) 48,538 wa majisafi kutoka maunganisho 4,800 yaliyokuwepo wakati inaanzishwa mwaka 1998. Mafanikio katika ongezeko hili la maunganisho

limetokana na uwekezaji mbalimbali wa miradi ya majisafi na majitaka uliofanywa na Serikali na DUWASA yenyewe ikiwa ni pamoja na mikopo toka taasisi za fedha. Grafu ifuatayo inaonesha mgawanyiko na aina ya wateja (*customer categories*) wa DUWASA.




## 3.2 Huduma ya Majitaka

### 3.2.1 Mfumo wa kukusanya na kusafirisha majitaka

Mnamo mwezi Februari 2002, DUWASA ilikabidhiwa dhamana ya kuendesha na kuhudumia mfumo wa majitaka mjini Dodoma kutoka CDA ambapo jumla ya wateja wapatao 2,000 walikuwa wamejiunga. Mpaka sasa mtandao una urefu wa km **113.7km** (Juni, 2020) ambao unajumuisha mabomba makubwa ya kusafirishia majitaka (*trunk sewer & sub trunk*) yenye kipenyo cha mm 1100 na urefu wa km 24.3 na (*lateral sewers*) wenye jumla ya urefu wa km 89.4 Mtandao huu unajumuisha pia eneo la ndani ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Mtandao mkuu wa kusafirishia majitaka (*Main trunk*) umesanifiwa kuhudumia watu wapatao 423,000. Hata hivyo, mtandao huu unahudumia takribani asilimia 20 tu ya wakazi kutokana na ukosefu wa mitandao midogo ya mabomba ya kukusanyia majitaka (*lateral sewers*).

Mitandao ya kukusanyia majitaka imeenea kikamilifu (*comprehensive reticulation sewers network*) kwenye maeneo matatu tu ya mji. Maeneo hayo ni Mlimwa West (Area C), Mlimwa *East* (Area D) na *Central Business Area*. Maeneo mengine ya mji yaliyofikiwa na mtandao wa kukusanyia majitaka japo kwa kiasi kidogo ni kata za Makole, Viwandani, Madukani, Kizota, Chamwino, Kikuyu Kaskazini, Uhuru na Tambukareli.

Kwa maeneo ambayo mtandao wa majitaka haujafikia, wananchi wamekuwa wakitumia njia za *septic* na *soak pit*. DUWASA ina gari maalum la kunyonya majitaka *(Cesspit emptiertruck)* ambalo hutumika kuhudumia maeneo hayo yasiyo na mfumo wa uondoshaji majitaka. Huduma hii pia hutolewa na Jiji pamoja na watu binafsi.

Hadi sasa, DUWASA ina jumla ya maunganisho (wateja) 5,935 ya majitaka kutoka maunganisho 2,000 yaliyokuwepo wakati inakabidhiwa mfumo wa Majitaka mwaka 2002.

### 3.2.2 Mabwawa ya kutibu Majitaka

Mfumo uliopo wa kutibu majitaka ni mabwawa (*Waste Stabilization Ponds - WSPs*) yaliyopo kilometa zipatazo sita (6) toka mjini. Mabwawa haya yapo manne (4) kila moja likiwa na ukubwa wa meta 200 X 200. Mabwawa haya yalisanifiwa kwa muda ili kuhudumia watu 68,000 tu. Kwa sasa mabwawa haya yamezidiwa kutokana na kuhudumia watu wanaozidi usanifu wake. Mpango wa kujenga mabwawa mengine ya kudumu katika eneo la Nzuguni upo katika hatua ya kutafuta fedha za ujenzi.



*Mabwawa ya kutibu majitaka yaliyopo Swaswa*

### 3.2.3 Upimaji wa ubora wa majisafi na Majitaka

DUWASA hutumia maabara yake kupimia ubora wa majisafi na majitaka. Sampuli za majisafi kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya mjini huchukuliwa na kupimwa mara mbili (2) kila mwezi ambazo hujumuisha *physical*, *Chemical* pamoja na *Bacterilogical parameters*. Vilevile, sampuli za majitaka huchukuliwa na kupimwa toka katika mabwawa ya kutibu majitaka mara mbili (2) kila mwezi.

Kwa mujibu wa matokeo ya vipimo vya majisafi, maji yanayozalishwa na kusambazwa na DUWASA ni safi na salama kwa matumizi ya binadamu. Hii huthibitishwa pia na EWURA ambayo kwa wakati wake hufanya upimaji wa ubora wa majisafi katika maeneo mbalimbali ya mji na kuridhika kuwa ni safi na salama. Aidha, DUWASA huchukua sampuli za maji na kuzipeleka kwenye maabara zingine mara mbili kwa mwaka ili kulinganisha matokeo ya ubora wa maji.

Kwa upande wa majitaka, hali ya ubora wa majitaka yanayotoka kwenye mabwawa yaliyopo Swaswa hayakidhi viwango vya ubora unaotakiwa kutokana na kuzidiwa kwa uwezo wa kutibu wa mabwawa hayo. Mabwawa yaliyopo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) yamesanifiwa kuweza kutibu majitaka ya chuo kizima na maeneo ya jirani. Hadi sasa Mabwawa hayo yanafanya kazi vizuri.

## 4.0 UCHAKATAJI WA ANKARA, USAMBAZAJI NA MALIPO (MAKUSANYO)

### 4.1 Uchakataji wa Ankara na Usambazaji


Uchakataji wa Ankara kwa wateja wote wa DUWASA hufanyika kwa kutumia mfumo wa *Smart Billing Manager-(SBM)*. Wasoma mita hukusanya *readings* kutoka kwa wateja kwa kutumia *mobile application* ambapo usomaji huingizwa katika *System* moja kwa moja ambayo hutengeneza Ankara *automatically*. Utengenezaji wa Ankara hufanyika tarehe 21 ya kila mwezi.

### 4.2 Makusanyo

Tangu mwezi Februari, 2018, DUWASA ilianza kukusanya malipo ya Ankara kutoka kwa wateja kwa kutumia mfumo wa kieletroniki wa Serikali (*Government Electronic Payment Gateway, GePG*) kupitia simu za mkonomi mitandao ya TTCL, Vodacom, Tigo, Airtel na Halotel pamoja na benki za NMB, CRDB, NBC pamoja na Wakala zake. Wakati huo, malipo ya fedha taslimu pia yaliendelea kupokelewa katika vituo viwili vya DUWASA vilivyokuwa Ofisi kuu na ofisi ya RAS. Hata hivyo, ilipofika mwezi Mei, 2018, DUWASA ilisitisha rasmi malipo ya fedha taslimu na kufunga vituo vyote viwili vilivyokuwa vikitumika kupokelea fedha taslimu. Hivyo, kuanzia mwezi Mei, 2018, malipo yote ya Ankara yanapokelewa kupitia mfumo wa *GePG*. DUWASA ilikuwa Mamlaka ya kwanza ya maji kuanza kutumia mfumo wa kukusanya mapato wa Serikali (GePG) ambao upo kwa mujibu wa sheria.

Aidha, DUWASA inasambaza Ankara za wateja wa majumbani kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu isipokuwa wateja wa Taasisi na Wateja wakubwa wa biashara ambao bado wanapelekewa Ankara zao za kudurufu. Kwa sasa wastani wa Shs. 1.5m/= hadi 1.7Bn/= hukusanywa kila mwezi kutoka wastani wa Shs. 14m/- kwa mwezi wakati DUWASA inaanzishwa mwaka 1998. Mafanikio haya yametokana

na kutekeleza miradi ya ujenzi wa mitandao ya usambazaji maji hivyo kuongeza maunganisho. *Graph* ifuatayo inaonesha *trend* ya makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.




## 5.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI DUWASA

Baadhi ya changamoto zinazoikabili DUWASA katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ni pamoja na: -

- Ongezeko kubwa la watu baada ya Serikali kuhamia Dodoma, hivyo kuongeza mahitaji ya maji
- Ufinyu wa mtandao wa kusambazia majisafi ambapo, zaidi ya kilometa 400 zinahitajika kujengwa ili kuyafikia maeneo mapya yasiyo na mitandao na yale yanayoendelea kuendelezwa. Pia urefu wa mtandao wa majitaka ni kilometa 113 tu ikilinganishwa na takribani kilometa 250 zinazohitajika.
- Upotevu wa maji unaofikia wastani wa 27% hali ambayo bado haijafikia kiwango cha 20% kinachokubalika. Juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanyika na kuweza kupunguza kutoka wastani wa 40% mwaka 2010.
- Kubomoka kwa mitandao ya majitaka iliyojengwa kwa zege kwenye maeneo ya Area C na D, hivyo kusababisha mfumo wa kusafirisha majitaka katika maeneo hayo kuziba mara kwa mara na kutoa harufu mbaya. Katika maeneo hayo, jumla ya km zipatazo 19 zimekwishakuwa dhaifu na zinatakiwa kubadilishwa kwa gharama ya Shs 4.5bn/=.
- Wizi wa Maji unaofanywa na baadhi ya wateja wasio waaminifu hali inayosababisha upotevu wa maji na kuikosesha DUWASA mapato ya kuweza kujiendesha na kuhudumia wananchi kwa hali endelevu. Kwa Kipindi cha Januari hadi Juni 2020, jumla ya Wateja 217 walikutwa na makosa mbalimbali yaliyoashiria uwepo wa wizi wa maji.

## 6.0 MIPANGO YA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA JIJINI DODOMA

### 6.1 Mipango ya muda mfupi na muda mrefu

Mipango ifuatayo imepangwa kutekelezwa na DUWASA kwa kushirikiana na Serikali (Wizara ya Maji na Washirika wa Maendeleo katika Sekta ya maji). Aidha mipango mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na mingine inatarajiwa kuanza. Umuhimu wa kutekeleza mipango hii unasukumwa kwa kiasi kikubwa na uamuzi wa Serikali ya awamu ya tano (5) kuhamia Makao Makuu ya Nchi – Dodoma. Kuhamia kwa Serikali Dodoma kumesababisha ongezeko la uhitaji wa huduma nyingi za kijamii ikiwemo huduma nyeti ya maji ambayo imekuwa ikiongezeka kwa kasi siku hadi siku.

#### 6.2.1 Mipango ya muda mfupi na inayoendelea

Mipango ifuatayo inaendelea kutekelezwa na DUWASA na mingine inatarajiwa kuanza katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja ujao.

**(a) Miradi ya kusambaza maji maeneo yasiyo na huduma**

Katika kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa mitandao ya kusambazia majisafi ili kuyafikia maeneo yasiyo na huduma, DUWASA inaendelea na utekelezaji wa miradi midogo ya kusambaza maji katika maeneo ya Mlimwa *Hill*, Michese, Mkalama, Mkonze, Ntyuka kwa kutumia uwezo wake wa ndani.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, DUWASA ilitenga Shs. 2.02Bn/= kwa ajili ya kusogeza huduma ya maji kwenye maeneo haya. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, DUWASA imetenga jumla ya shilingi 2.2Bil/- na imepanga kukopa Shs. 1.5bn/= kupitia mfuko wa *Investiment Financing Facilities (IFF)* unaofadhiliwa na KfW kwa kushirikiana na Wizara ya Maji ili kuwezesha usambazaji maji katika maeneo mbalimbali Jijini.

**(b) Uchimbaji Visima pembezoni mwa Mji ili kupata vyanzo vingine vya maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma**

Kwa kutumia Bajeti yake pamoja na msaada wa Wizara ya Maji, DUWASA inatumia DDCA kuchimba visima kwenye maeneo ya Ntyuka, Zuzu, Michese na maeneo ya chuo cha Mipango ambayo Wataalam kutoka Idara ya Rasilimali maji (MoW) wamepima na kubaini uwezekano wa kupata maji chini ya Ardhi.

Uchimbaji visima umeanza kwa eneo la Ntyuka na Zuzu ambapo, kwa eneo la Ntyuka, uchimbaji umekamilika lakini wachimbaji hawakuweza kupata maji licha ya kufikia kina cha mita 192 chini ya ardhi, utafiti zaidi utafanyika eneo hilo ili kuweza kupata maji. Aidha, uchimbaji eneo la Zuzu umefanyika kwa kuchimba kisima kimoja kati ya vitatu vinavyotarajiwa kuchimbwa katika eneo hilo. Kisima hicho kimebainika kuwa na maji mengi (takribani 40m3/hr) na mazuri kwa matumizi ya binadamu. *Pumping test* ya kisima cha Zuzu itafanyika baadaye ili kufahamu uwezo halisi wa Kisima hicho. Kwa sasa DDCA wapo eneo la Chamwino Ikulu ambapo wanaendelea na uchimbaji wa visima, na pindi watakapokamilisha wataendelea kwenye maeneo mengine ikiwemo Ihumwa, Zuzu, Michese, na Mpamaa.

**(c) Utafiti wa maji chini ya Ardhi, Uchimbaji na uendelezaji wa Visima kumi katika Mji wa Chamwino.**

Ili kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Chamwino, Wizara iliielekeza DUWASA kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na kuchimba visima vinavyoweza kutoa maji ya kutosheleza mahitaji ya maji ya Mji wa Chamwino.

DUWASA iliingia Mkataba na DDCA wa kufanya utafiti wa *sites* 10 katika Mji wa Chamwino na kuchimba visima vinane kwa jumla ya shilingi 456,236,000/-. DDCA wamekamilisha uchimbaji wa visima nane (8) kati kumi (10) ambavyo vimebainika kuwa na maji mengi. Hata hivyo, Visima vitatu (4) kati ya hivyo vina maji ya chumvi inayozidi kiwango kinachoruhusiwa. Hivyo, DUWASA inatarajiwa kuvitumia visima hivyo kwa kuchanganya maji yake na visima ambavyo havina chumvi (*blending*) ili kupata maji yenye ubora unaotakiwa. DUWASA imewasilisha andiko maalumu Wizara ya Maji la kuomba fedha (11Bil/-) kwa ajili ya kutekeleza mipango ya muda mfupi ya kuboresha huduma ya maji Jijini Dodoma na Chamwino. Wizara ya Maji imeukubali ushauri wa DUWASA.

**(d) Miradi ya upanuzi wa mtandao wa Majitaka**

DUWASA kwa kutumia uwezo wake wa ndani imetekeleza mradi wa Majitaka eneo la kigamboni umbali wa mita 750 kwa kulaza mabomba ya kipenyo cha milimita 250(10”) ambapo imegharimu jumla ya shilingi milioni 57. Wateja zaidi ya 33 ambao wapo karibu na Mtandao huo uliojengwa watanufaika.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, DUWASA imetenga jumla ya shilingi 546mil/- kwa ajili ya kutekeleza miradi ya majitaka kwenye maeneo ya Chamwino (Bonanza), Swaswa, Bahiroad (mtaa wa Kitenge) Chang’ombe, Area A na Kinyambwa.

### 6.2.2 Mipango ya muda wa kati

Kazi zifuatazo zinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu ili kuwa na uhakika wa huduma ya majisafi na uondoshaji majitaka Jijini Dodoma.

**(a) Mradi wa Chanzo cha Maji cha Farkwa –Wilaya ya Chemba**

Mradi wa ujenzi wa Bwawa la maji katika tarafa ya Farkwa iliyopo wilaya mpya ya Chemba una lengo la kupata chanzo cha nyongeza cha maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma Pamoja na Wilaya za Chemba, Bahi na Chamwino. Kazi ya tathmini ya athari za mazingira na kijamii (ESIA) zinazofanywa na Mtaalam mshauri *Tres Consult ltd* kutoka Tanzania zimekamilika na Baraza la Mazingira (NEMC) limetoa kibali cha kujengwa kwa Bwawa hilo. Aidha, kazi za usanifu wa kina zilizofanywa na Mhandisi Mshauri *M/S TRACTEBEL Engineering* kutoka Ufaransa zimekamilika. Mnamo mwezi Desemba, 2019, Serikali kupitia Wizara ya Maji ililipa fidia ya jumla ya shilingi 7.6 Bil/- kwa Wananchi wanaoathirika na ujenzi wa Bwawa hilo.

Mradi huu unasimamiwa na Wizara ya Maji ambapo pamoja na matumizi mengine ya bwawa, utekelezaji wa mradi utawezesha ongezeko la maji mjini Dodoma kwa meta za ujazo 128,000 kwa siku. Kiasi hiki kinatosheleza mahitaji ya maji ya watu zaidi ya milioni moja (1,000,000). Wizara ya Maji inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa hilo.

**(b) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uondoshaji na kutibu majitaka Mjini**

DUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji ina mpango wa kutekeleza mradi mkubwa wa Majitaka ambao utagharimu Dola za marekani Milioni 70. Mradi huo utafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Korea. DUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ziko kwenye hatua nzuri ya majadiliano kuhusu kupatiwa mkopo huo ambao umepangwa kutumika kujenga mabwabwa mapya (WSP) ya kutibu Majitaka katika eneo la Nzuguni na kulaza mabomba ya kukusanyia majika kwenye maeneo mbalimbali.

Tayari DUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji imeshapata eneo la ujenzi wa mabwawa mapya ya kutibu majitaka katika eneo la Nzuguni na jmla ya shilingi Milioni 611 zimetumika katika ulipaji wa fidia kwa ajili ya eneo hilo la mabwawa lenye ukubwa wa hekta 60.

### 6.2.3 Mpango wa muda mrefu

**(a) Mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria**

Mpango wa muda mrefu ni ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka ziwa Victoria hadi Dodoma. Mradi huu utahudumia pia Mji wa Singida na miji mingine iliyopo njiani. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kufanyika kwa *Pre-Feasibility Study* ambayo ilikamilika mwezi Desemba, 2019 kwa

kutumia Wataalamu wa Wizara ya Maji (Wizara, Mamlaka na Mabonde). Matokeo haya ya awali yameonesha kuna uwezekano wa maji kutoka Ziwa Victoria na kufika Dodoma. Kwa sasa hatua inayofanyika ni kufanya *Detailed Feasibility Study* na *Design* ambapo Wizara ya Maji itatangaza zabuni na kuajiri Mhandisi Mshauri atakayeandaa Usanifu wa kina na vitabu vya zabuni. Mradi huu unakadiriwa kugharimu zaidi ya Shilingi Trilioni 1.

## 7.0 HITIMISHO

- DUWASA itaendelea kufanya kila linalowezekana kuhakikisha wananchi wa Dodoma wanapata maji.
- DUWASA inaiomba Serikali iendelee kuiangalia Dodoma kwa jicho la pekee kwa kuwa Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi na Serikali imeshahamia Dodoma.

Naomba kuwasilisha,

Eng. David T. Pallangyo

**MKURUGENZI MTENDAJI**